

Henoch-Schönlein Purpura (Swahili)

Henoch-Schönlein Purpura (HSP)



Henoch-Schönlein Purpura (HSP) ni hali ambapo mishipa midogo ya damu mwilini (hasa katika ngozi, utumbo, na mafigo) huumia na kuvimba na kusababisha upele. HSP ni kawaida katika watoto wa umri wa miaka 2 hadi 8. HSP inaweza kuanzishwa na virusi kama mafua au homa ya mafua. Haiwezi kuenezwa kwa watu wengine.

Ishara na dalili



Upele ulioinuka na madoa mekundu-zambarau kwenye matako, miguu na viwiko



Maumivu kwenye tumbo



Mikono na miguu iliyovimba



Damu katika choo au mkojo wa mtoto wako



Maumivu katika viungo (kawaida katika magoti au vifundo vya miguu)

Je, inatambua jinsi gani?

Hakuna kipimo kwa HSP. Daktari wako anaweza kutambua HSP kwa kuangalia upele kwenye ngozi ya mtoto wako na kuuliza kuhusu dalili nyingine.

Daktari wako atapima shinikizo la damu la mtoto wako na kupata sampuli ya mkojo (kojo) ili kupima protini na damu katika mkojo. Anaweza pia kufanya kipimo cha damu ili kuangalia mafigo.

Matibabu

Maumivu madogo	Maumivu ya kati	Maumivu makali
<p>Mpe dawa ya kupunguza maumivu kwa mtoto wako</p> <p>Hakikisha mtoto wako anapumzika</p> <p>Weka miguu ya mtoto wako juu</p>	<p>Mtoto wako anaweza kuhitaji matibabu ya steroidi (zungumza na daktari wako kuhusu chaguo hili la matibabu)</p>	<p>Mtoto wako anaweza kuhitaji vipimo zaidi na huenda anahitaji kulazwa hospitali</p>

Watoto wengi watapata nafuu kutokana na HSP ndani ya wiki 4, na maumivu ya viungo yanatarajia kuondoka baada ya siku 3 za kwanza. Ni kawaida kwa dalili kurudi ndani ya miezi michache ya kwanza kwa baadhi ya watoto. Walakini, dalili hazitakuwa mbaya sana.



Utunzaji wa nyumbani

- Hakikisha kuwa mtoto wako anakunywa majimaji ya kutosha ikiwa ni pamoja na maji.
- Mpe paracetamol (Panadol au Dymadon) na ibuprofen (Nurofen) ili kusaidia kupunguza maumivu. Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kipimo cha sahihi. Usimpe mtoto wako kipimo zaidi ya kile kinachopendekezwa kwa siku.

Kwa ushauri wa matibabu usio wa dharura, piga simu 13 HEALTH (13 43 25 84) kuzungumza na muuguzi aliyesajiliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa gharama ya simu ya mtaa. Omba kupata mkalimani ikiwa unamhitaji.

Miadi ya kufuatilia

Mtoto wako atahitaji kuchunguzwa mara kwa mara na daktari kwa muda wa miezi 6 hadi 12 baada ya kugunduliwa, ikiwa ni pamoja na vipimo vya mkojo (kojo) na kupima shinikizo la damu. Hii ni kuhakikisha mtoto wako hana matatizo ya mafigo. Tafadhali weka miadi na daktari wako ili kuanza ukaguzi huu haraka iwezekanavyo - tumia ratiba ya miadi iliyo hapa chini.

Ikiwa mtoto wako ana matatizo ya figo baada ya miezi 3, daktari wako atamtuma kwa mtaalamu.

Ratiba ya miadi			
Wakati	✓	Wakati	✓
Wiki 1		Wiki 10	
Wiki 2		Wiki 12 (mtoto wako atatumwa kwa mtaalamu ikiwa matatizo ya figo yatagunduliwa)	
Wiki 3			
Wiki 4		Miezi 6	
Wiki 6		Miezi 9	
Wiki 8		Miezi 12 (na kisha kila mwaka)	

Wakati wa kuonana na daktari

Mwona GP wako ikiwa mtoto wako ana:



maumivu au uvimbe wa viungo



maumivu ya tumbo



damu katika choo au mkojo wake.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi.

Resource ID: FS135 **Reviewed:** July 2022 **Kanusho:** Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.